ISSN 0856 – 034X

Supplement No. 19 *10th May, 2019*

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 19 Vol 100 dated 10th May, 2019

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 390 la tarehe 10/5/2019

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO, MAGULIO NA MINADA ZA HALMASHAURI YA WILAYA MPIMBWE ZA MWAKA 2019

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko, Magulio na Minada za Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe za Mwaka 2019.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelekezwa au kufafanuliwa vinginevyo:-

"Afisa Masuuli" maana yake ni Mkurugenzi au afisa yeyote atakayekuwa anakaimu nafasi ya Mkurugenzi;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake afisa yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe;

"mfanyabiashara" maana yake ni mfanyabiashara yeyote anayeuza bidhaa katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na mfanyabiashara ndogondogo au machinga;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakaye kuwa anatekeleza majukumu ya Mkurugenzi kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"soko" maana yake ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko,

"taka" maana yake ni taka ngumu, taka maji au kimiminika pamoja na taka laini,

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru au ada kwa niaba ya Halmashauri,

Ushuru wa soko, mnada na gulio

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa kila biashara inayofanyika katika eneo lililoainishwa na Halmashauri kama soko, gulio au mnada.

(2) Ushuru wa soko, gulio au mnada utatozwa na Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hii.

Namna ya kukusanya Ushuru wa soko, gulio au mnada

5.-(1) Bila kuathiri masharti ya Kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hii, Halmashauri itaweka utaratibu wa kukusanya ushuru wa masoko, gulio na minada kwa kadri itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga au kuainisha maeneo maalum yatakayotumika kama masoko, minada au magulio.

(2) Malipo ya ushuru wa soko, gulio au mnada yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

(3) Halmashauri au Wakala itakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo mtu huyo ameshindwa kulipa ushuru wa soko au mnada ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(5) Endapo mali au bidhaa iliyokamatwa na Halmashauri

au Wakala haitalipiwa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa aliyekuwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ushuru unaodaiwa, gharama za Mahakama, ukamataji, utunzaji na uuzaji.

(6) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Afisa Masuuli.

Wajibu wa kulipa ushuru wa soko, gulio au mnada

6. Kila mfanyabiashara katika eneo la ushuru wa soko, gulio au mnada atakuwa na wajibu wa:

(a) kulipa kiwango cha ushuru kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa ushuru;
(c) kutunza kumbukumbu za malipo..
(d) kuweka eneo lake katika hali ya usafi.

Muda wa biashara

7.- (1) Kila soko, gulio au mnada litafunguliwa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa moja kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), mnada au gulio litafanyika kwa siku na maeneo ambayo yatapangwa na Halmashauri.

Uteuzi wa Wakala

8. Halmashauri inaweza kuteau kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru wa masoko, magulio au minada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Uwezo wa Afisa Mwidhini wa

9. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote la soko,mnada au gulio kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tatimini au kufanya jambo lolote linalohusu ushuru wa soko, gulio au mnada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Mamlaka ya Halmasha

10. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Halmshauri itakuwa na mamlaka ya kutoa mwongozo kuhusu

uri kutoa Mwongozo utaratibu wa kuendesha soko, gulio au mnada endapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

Makosa

11. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii endapo mtu yeyote:-

(a) atashindwa kulipa ushuru;

(b) atashawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ushuru wa soko, gulio au mnada;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa ada au ushuru;

(e) atashindwa kuweka eneo lake la biashara katika mazingira ya usafi;

(f) atatupa au kuweka taka katika eneo lisiloruhusiwa katika soko, gulio au mnada;

(g) ataanzisha soko, gulio au mnada katika eneo ambalo halijaruhusiwa na Halmashauri; au

(h) atauza bidhaa katika eneo la mnada au gulio katika siku ambayo haijaainishwa na Halmashauri kama siku ya mnada au gulio.

Adhabu

12. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Kifungu cha 11 atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 4(2))

SEHEMU YA KWANZA

Ushuru wa Soko, Minada na Gulio:

A. Ushuru wa Bidhaa kwenye Minada

Na.	*Aina ya Bidhaa*	*Kiwango cha Ushuru (Tshs)*
1.	Nguo	1,500/= kwa siku
2.	Bia na Vinywaji Baridi	1,500/= kwa siku
3.	Pombe za Asili	1,500/=kwa siku
4.	Dawa za Asili	1,500/=kwa siku
5.	Nyama	1,500/=kwa siku
6.	Vyombo vya Nyumbani	1,500/=kwa siku
7.	Viatu	1,500/=kwa siku
8.	Nyingine	1,500/= kwa siku

B. Ushuru wa bidhaa katika masoko yaliyotengwa na Halmashauri :

Na	*Aina ya Biashara/Bidhaa*	*Ushuru/Kodi ya Pango*	*Muda*
1.	Vibanda	kwa mujibu wa mkataba.	
2.	Meza	Tshs. 200/= kwa meza	Kwa siku
3.	mitumba	Tshs 500/=	Kwa siku
4.	Nguo za madukani kutandaza	Tshs. 500/	Kwa siku
5.	Ndizi za kupika mkungu	Tshs. 200/=	Kwa siku
7.	Ndizi mbivu mkungu	Tshs. 200/=	Kwa siku
8.	Nanasi (tenga)	Tshs. 500/=	Kwa siku
9.	Maparachichi (tenga)	Tshs. 500/=	Kwa siku
10.	Mboga-mboga (tenga)	Tshs. 200/=	Kwa siku
11.	Nyanyanyanya mshumaa (tenga)	Tshs. 300/=	Kwa siku
12.	Machungwa (tenga)	Tshs. 200/=	Kwa siku
13.	Viatu vya mitumba	Tshs.1,000/=	Kwa siku
14.	Mama au Baba lishe	Tshs.500/=	Kwa siku
15.	Vyombo vya ndani	Tshs.500/=	Kwa siku

16.	Nyama au nyama choma	Tshs. 1,000/=	Kwa siku
17.	Urembo	Tshs.500/=	Kwa siku
18.	Bidhaa mchanganyiko	Tshs.500/=	Kwa siku
19.	Samani (furniture)	Tshs. 5,000	Kwa mwezi
20.	Vyungu	Tsh 500/=	Kwa siku
21.	Miwa	Tsh 500/=	Kwa siku
22.	Bia na soda	Tsh 1,000/=	Kwa siku
24.	Dawa ya asili	Tsh 500/=	Kwa siku
25.	Nyingine	Tshs.500/=	Kwa siku

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

(Limetengenezwa Chini ya Kifungu cha 13)

Mimi …….. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …….. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, kwamba Tarehe …….. ya Mwezi …….Mwaka …….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …….. cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko, Magulio na Minada ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ya Mwaka 2019.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi……badala ya kushtakiwa Mahakamani na nipo tayari kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe …….. ya Mwezi …… Mwaka ……

Jina ……

Saini ……

Mbele ya:

Jina …….. Cheo …….

Saini ……

Nembo ya Halmashauri Wilaya ya Mpimbwe imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 26/01/2018 mbele ya:-

ERASTO N. KIWALE

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe

L.S

NYANSONGO M.SERENGETI
Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe

NAKUBALI

Dodoma,
29 Machi, 2019

SELEMANI S. JAFO, (Mb)
Waziri wa Nchi- OR-
TAMISEMI